# HALMASHAURI YA WILAYA YA MALINYI

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 17/11/2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MALIYI

**1.00 MAHUDHURIO:**

**1.01 Wajumbe waliohudhuria:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. Pius Mwelase | Mwenyekiti H/W | Mwenyekiti |
| 2. | Mh. Said Tira | Diwani Kata ya Malinyi | Mjumbe |
| 3. | Mh. Severus A. Kamguna | Diwani Kata ya Igawa | Mjumbe |
| 4. | Mh. Editha A. Makumba | D/V/M Ngoheranga | Mjumbe |
| 5. | Mh. Bonaveture Kiwanga | Diwani Kata ya Kilosampepo | Mjumbe |
| 6. | Mh. Jane Komba | Diwani Kata ya Mtimbira | Mjumbe |
| 7. | Mh. Lucas Mgomahenga | Diwani Kata ya Sofi | Mjumbe |

**1.02 WAKUU WA IDARA NA WAGENI WAALIKWA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | JoanFaith Kataraia | Mkurugenzi Mtendaji (W) | Katibu |
| 2. | George Lazaro | K/Mkuu wa Idara ya U/Utawala | Mjumbe |
| 3. | Simon Nkwabi | K/Mkuu wa Idara ya U/Zimamoto | Mjumbe |
| 4. | Sarah Kibona | K/Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara | Mjumbe |
| 5 | Joseph C.Nyange | K/Mkuu wa Idara ya K/U/Ushirika (W) | Mjumbe |
| 6 | Hermina Mbele | K/Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA | Mjumbe |
| 7 | Feddy Munyaga | Mkuu wa idara ya Ardhi na Maliasili | Mjumbe |
| 8 | Seuri Laizer | K/Mkuu kitengo cha Sheria | Mjumbe |
| 9 | Emil Kalanga | Mkuu wa Kitengo cha uchaguzi | Mjumbe |
| 10 | Absalom Gepson | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi | Mjumbe |
| 11 | Tumaini Bwire | K/Mkuu wa Kitengo cha Nyuki | Mjumbe |
| 12 | Omary Seif | KMkuu wa Idara ya M/Jamii | Mjumbe |
| 13 | Gabriel Masejo | K/Mkuu Kitengo cha Manunuzi | Mjumbe |
| 14 | Dr. Aziz Keto | K/Mganga Mkuu (W) | Mjumbe |
| 15 | Ntuli Mwakabungu | Mkuu wa Idara ya E/Sekondari | Mjumbe |
| 16 | Linda Marandu | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi | Mjumbe |
| 17 | Lewis Mcharo | K/Mkuu wa Kitengo Ukaguzi wa Ndani | Mjumbe |
| 18 | Christina C.Chacha | Mkuu wa Idara ya Mazingira | Mjumbe |
| 19 | Deus Nyoni | Mkuu wa Idara ya Mipango | Mjumbe |
| 20. | Sylivia Lusumo | Mratibu wa TASAF | Mjumbe |
| 20 | Christina C. Sulley | Kaimu Katibu TSC | Mwalikwa |

**1.03 SEKRETARIETI**

1. Issa Matanda — Mwandishi wa vikao
2. Kimwana Mwatawala — Mwandishi wa vikao

**KUMB.NA. 01/11/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliwakaribisha wajumbe katika kikao na kumtaarifu Mwenyekiti kuwa akidi imetimia hivyo afungue kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa mahudhurio mazuri na kuwataka kuwa huru katika kuhoji na kupata majibu yaliyo sahihi.

Mwenyekiti alifungua kikao saa **05:20** asubuhi.

**KUMB.NA. 02/11/2021: KUTHIBITISHA AGENDA**

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia agenda na kuzithibitisha, wajumbe walizithibitisha agenda zifuatazo zijadiliwe katika kikao.

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 20/10/2021
4. Yatokanayo na kikao cha tarehe 20/10/2021
5. Taarifa ya Mapato na Matumizi mwezi Oktoba,2021
6. Taarifa za kiutumishi
7. Taarifa ya mapokezi ya Fedha za ujenzi wa Madarasa 44 Elimu Msingi kutoka Serikali Kuu.
8. Mengineyo
9. Kufunga kikao.

**KUMB.NA.03/11/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 20/10/2021**

Wajumbe waliusoma muhtasari wa kikao cha tarehe 20/10/2021 kilichopita na kuridhia Katibu na Mwenyekiti kusaini.

**KUMB.NA.04/11/2021: YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 20/10/2021**

Suala la kumpata mkusanya ushuru kivuko cha Ngombo Mto Mnyera, suala hili limetekelezwa na taarifa imetolewa.

**AGIZO TENA**

Suala la kukatia Bima mtambo wa Shindilia la Halmashauri, mtaalamu ameenda Ulanga kushughulikia suala la malipo.

Kuhusu kununuliwa viti getini Luvili, viti 8 vilinunuliwa na vipo katika eneo husika vinatumika.

**MAJADILIANO**

Diwani wa Kata ya Malinyi alitaka kujua kama taratibu zote zimefuatwa na pia alitaka majina yote ya watu walioomba nafasi ya ukusanyaji ushuru wa kivuko yawasilishwe mbele ya kikao.

Mkuu wa Idara ya Utumishi alieleza kuwa huo ni mchakato wa kitaalamu umepitia hatua mbalimbali hadi kumpata aliyeshinda. Kuwasilisha majina yote ni kuanza mchakato upya ambayo siyo kazi ya kamati ni kazi ya Bodi ya Ajira. Alimthibitishia mjumbe kuwa kazi hii imefanywa kwa uwazi na ikihudhuriwa na viongozi toka mkoani.

Wajumbe walijadili kwa kina na kubaini kuwa kazi ilifanyika kwa uwazi, hivyo walikubaliana kwa pamoja kuipokea na kuipitisha taarifa ya mchakato wa kumpata mkusanya ushuru wa kivuko cha mto Mnyera na Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira.

**KUMB.NA.07/11/2021: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA UJENZI WA MADARASA 44 ELIMU MSINGI KUTOKA SERIKALI KUU**

Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha jumla ya **Tsh 880,000,000/=** kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 44 katika shule shikizi 11 za msingi. Aidha taarifa ilionesha wakandarasi wawili wamepatikana wa kujenga madarasa hayo ambao ni

1. Mhandisi Ernest E. Elvica madarasa 15 katika vituo Shikizi (Salatogo, lumbanga na kitiliwele)
2. Mhandisi Joram Shabani Kiongo madarasa 29 ya shule shikizi za Madega B, Salamiti, Njasa, Mwambike, Mkanga, Ifugira Likea na Luvili.

Wajumbe waliipiia taarifa hiyo na kuijadili.

Wajumbe walisema kuwa hawajashirikishwa kwenye mchakato huu wa kuwapata wakandarasi watakaojenga madarasa hayo pia hawatambui kamati teule iliyopo kwani hawana taarifa yeyote kutoka Ofisi ya Mkurugenzi.

Baada ya majadiliano ya mda mrefu wajumbe waliagiza mchakato wa kuwapata wakandarasi urudiwe na kwa kuwa muda hautoshi kiitishwe kikao cha dharura kujadili kuwapata wakandarasi hao.

**KUMB.NA.08/11/2021: MENGINEYO**

Mjumbe kutoka kata ya Igawa aliomba kubadilishwa kwa mtendaji wa Kijiji aitwaye Faya kwani amekuwa ni kikwazo katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mjumbe huyo pia alizungumzia suala la uhamisho wa mwalimu wa sayansi kutoka shule ya sekondari Igawa na hakuna mwalimu aliyepelekwa kuziba nafasi hiyo.

Aliendelea kueleza kuwa mwalimu aliyepangiwa kwenda kuziba nafasi hiyo Mkuu wa Wilaya Ndugu Mathayo Masele inasemekana amemkataza kwenda kuripoti shuleni Igawa hali iliyopelekea waanafunzi kutofundishwa somo la Fizikia.

Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari alijibu kuwa utaratibu wa uhamisho uko palepale na asipotekeleza Ofisi ya TSC itachukua hatua za kinidhamu dhidi yake.

Mjumbe kutoka kata ya Malinyi alizungumzia suala la aliyekuwa mtumishi wa Halmashauri ya Malinyi Ndugu Jane Tiamaru arudishwe kazini na kama hana sifa aandikiwe barua ili ajulishwe.

**KUMB.NA.09/11/2021: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao ya mawazo kisha alifunga kikao saa 08:20 mchana.

**MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA NA:**

| | |
|---|---|
| **Saini:** ............... | **Saini:** ............... |
| **Jina:** NTULA A. MWAKALOBO | **Jina:** JANE O. KOMBA |
| **Katibu** | **Mwenyekiti** |
| **Tarehe:** 24/12/2021 | **Tarehe:** 24/12/2021 |